

# **Ushairi wa Kiswahili na Uwasilishaji wa Harakati za Kukabiliana na Matatizo Yaliyopo katika Mataifa Huru ya Afrika**

Joseph Nyehita Maitaria  
na  
Richard Makhanu Wafula

## ***Ikisiri***

*Makala haya yanafafanua namna ushairi wa kiharakati wa Kiswahili unavyobainisha na kukabiliana na matatizo yaliyopo kwa sasa katika baadhi ya mataifa huru ya Afrika. Kinaudhui, kuma makundi mawili ya watunzi: wale wanaostahabu kubainisha matatizo hayo na wale wanaofanya hivyo na pia kutoa maelekezo katika kukabiliana na matatizo hayo. Kadhalika, lugha inayotumiwa katika uwasilishaji wa tungo huweza kuwa ya moja kwa moja au ya kitamathali. Kihistoria, baadhi ya matatizo hayo yalitokana na utawala wa ukoloni ulipokitwa barani Afrika. Majilio ya wageni hao na mifumo yao ya kiutawala ilisababisha utata na kuathiri mielekeo ya wenyeji kuhusu dhana ya ustaarabu na maendeleo katika tamaduni za jamii hizo. Baada ya uhuru, kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1960 hadi sasa, baadhi ya mataifa hayo yameyumba kutokana na sintofahamu ya jinsi ya kukabiliana na matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika mashairi teule, itabainishwa namna mbinu za kisanaa zilivyotumiwa katika kufichua kiini cha matatizo hayo na kuonyesha namna ya kukabiliana nayo. Kidole cha lawama pia kinaelekezwa kwa wenyeji. Mashairi yanayozingatiwa katika makala haya ni yale yanayopatikana katika diwani za A. Abdalla (1973), Sauti ya Dhiki; E. Kezilahabi (1974), Kichomi; A. Mazrui (1984), Chembe cha Moyo; S. A. Mohamed (2001), Jicho la Ndani na K. wa Mberia (2001). Makala pia, yatapendekeza namna ushairi wa Kiswahili unavyoweza kuboreshwa ili kuweza kutumiwa kwa ufaafu zaidi kama chombo cha kiharakati katika kukabiliana na matatizo hayo.*

## **1.0 Utangulizi**

Ushairi kama utanzu wa fasihi andishi ni sanaa inayobuniwa na kuwasilishwa kutokana na mazingira ambayo huakisi hali halisi katika jamii. Kwa hivyo, matukio yanayoshuhudiwa huwasilishwa kwa ubunifu katika muktadha wa utamaduni na historia ya jamii. Kupitia katika tungo hizo, falsafa na busara ya jamii huweza kufafanuliwa na kutumiwa katika kujenga mikakati ya kusuluhishia matatizo yaliyopo sasa. Kwa hivyo, uwasilishaji wa hisi na mielekeo ya kitiikadi inayoibuliwa katika utanzu wa ushairi ni ile inayotokana na tajiriba ya watu katika mazingira ya utamaduni wao. Kwa maana hiyo, utanzu wa ushairi wa Kiswahili unapigwa darubini ili kudhihirisha namna unavyowasilisha maudhui ya harakati

katika kukabiliana na matatizo yaliyopo katika baadhi ya mataifa huru ya Afrika. Baadhi ya matatizo ambayo yanahitaji suluhu ni kama vile ukosefu wa miundombinu katika kuutumua uchumi, utoaji wa huduma za kijamii, uozo wa jamii, uzembe wa serikali unaosababisha usalama kuzorota na mikakati ifaayo katika ukuzaji wa talanta miongoni mwa vijana.

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na umekuwa ukitumiwa kama chombo cha kuwasilishia masuala muhimu kuhusu uhalisi wa maisha katika jamii (Abdalla, 1978). Kabla ya majilio ya wageni kutoka Ulaya na mifumo yao ya utawala, ushairi huo ulikuwa ukitumika kama nyenzo ya burudani na ya kuwasilishia uhalisi wa matatizo yanayoshuhudiwa katika jamii. Kadhalika, mataifa huru ya Afrika yamekuwa yakijengewa mazingira ya kutambua matatizo yaliyopo na namna ya kukabiliana nayo. Kwa mfano, katika karne ya 19, kulikuwepo na washairi mahashumu walioweza kujifunga kibwebwe ili kubainisha uhalisi wa matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kupitia kwa lugha iliyotumika, jamii zimekuwa zikiwasilishiwa ama kwa uwazi au kwa mafumbo ili kuweza kusaili na kutafakari kuhusu asili au chanzo cha matatizo hayo. Miongoni mwa washairi maarufu wa Kiswahili wa hapo awali ni kama vile Ali Koti, Ahmed Nassir na Muyaka wa Muhaji. Kwa mfano, Muyaka wa Muhaji, aliwasilisha baadhi ya tungo zilizobainisha uhalisi, wa maisha katika jamii yake ya Mvita. Baadhi ya tungo hizo zilitumiwa kama chombo cha kuwazindua na kuwatanabahisha wenyeji kuhusu utawala wa Wareno (1500-1700) na Waarabu wa Omani ambapo utangamano wa wenyeji uliathiriwa na kuvurugwa. Kinachotambuliwa ni kuwa, tawala zote hizo zilikuwa zenye sura ya ukandamizaji ingawa baadhi ya wenyeji hawakuwa na ufahamu huo.

Katika wakati wa sasa kuna washairi tumbi wa Kiswahili wanaoendelea kunoa makali katika kuyapigia darubini masuala tenge ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Katika baadhi ya mataifa huru ya Afrika uangamizaji wa umaskini bado ni kitendawili. Miongoni mwa washairi hao wa kiharakati ni kama vile: Ahmed Nassir (Juma Bhalo), Mugyabuso M. Mulokozi na Kulikoyela K. Kahigi, Abdilatif Abdalla, Alamin Mazrui, Euphrase Kezilahabi, Said A. Mohamed na Kithaka wa Mberia. Kama wanaharakati wa uhamasishaji wa jamii, baadhi ya watunzi hao wamebainisha matatizo yaliyopo bila ya kupendekeza suluhu; wachache wao ndio waliojasiri kuwa katika mstari wa mbele kufichua kiini chake kwa azma ya kujenga msingi wa suluhu au tiba ya matatizo yaliyopo katika mataifa huru ya Afrika. Kwa mfano, mamilioni ya Waafrika hawawezi kugharimia mahitaji ya msingi. Aidha, ukosefu wa ajira, ardhi, mtaji wa kuwekeza, miundombinu, elimu ya kubabaisha, ufisadi, ukabila na ukosefu wa usalama ambayo ni baadhi ya msururu wa matatizo yanayotesa umma katika mataifa hayo ya Afrika. Kwa mujibu wa Mbaabu (1996), baadhi ya matatizo yanayoyazinga mataifa hayo yana chemchemi yake katika majilio ya wageni kutoka Ulaya na tawala zao za ukoloni zilizokitwa katika janibu hizo. Masikitiko ya Matheka (2013: 10) ni kwamba, ndoto ya mababu zetu ilikuwa ni kuwapo kwa taifa lenye

usalama, kuutokomeza ujinga na kuwapo kwa chachu za maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Hata hivyo, hayo yametumbukia nyongo kutokana na kushamiri kwa ufisadi katika asasi muhimu za umma na uelekezi usiofaa wa viongozi 'weusi' katika mataifa hayo. Katika kushadidia mawazo hayo, hakusita kubainisha ukweli mchungu kuwa mataifa hayo ya sasa ni ya 'mwenye nguvu mpishe' huku mnyonge akiendelea kuteseka na kukumbukwa tu wakati wa kupiga kura ambapo hudanganywa kwa ahadi bandia. Aidha, wanaowania kura hizo hujifanya 'wanakondoo' lakini wanapopata nyadhifa walizozihitaji, ngozi zao huanza kuwa zenye 'madoadoa ya chui' na kucha kuchipuza ikiwa ni ishara tosha ya kuparamia vile vilivyoundwa kwa jasho la wananchi. Baadhi ya matatizo hayo yamebainishwa na kutolewa suluhu katika tungo hizo ambapo wanajamii wote wanahitaji kuungana pamoja katika safari hiyo muhimu.

Katika kutathmini uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili kiharakati, makala haya yanafafanua mikufu miwili mikuu inayotumika: mkufu wa kimaudhui na mkufu wa kimtindo. Kadhalika, mkufu wa kimaudhui umegawanyika katika vipande viwili: mkufu wa kubainisha matatizo yaliyopo katika mataifa huru ya Afrika na mkufu unaobainisha na kuelekeza namna ya kukabiliana na matatizo hayo. Mkufu wa kimtindo kwa upande wake umegawanyika katika vipande viwili: matumizi ya lugha ya moja kwa moja na matumizi ya lugha ya kitamathali. Maudhui katika tungo za ushairi huweza kuwasilishwa kwa lugha iliyo wazi au ya kimaumbo (Gromov, 2006). Kwa kuzingatia mikufu hiyo, masuala yanayotatiza katika jamii na uhalisia wa matukio ya kihistoria yameweza kuhifadhiwa na kuwasilishwa kwa ubunifu kwenye tungo hizo. Hadhira finyu kwa pana ziliweza kuupata undani wa ujumbe unaowasilishwa kwa kuuhusisha na uhalisia wa yale yaliyoshuhudiwa katika mataifa yao. Isitoshe, mazingira ya kutathmini yaliweza kujengwa na hatua zinazopaswa kuchukuliwa zilidokezwa kimaumbo au kubainishwa wazi (Mulokozi, 1978). Hilo lilitegemea uhodari wa udhibiti wa lugha na kunga elekezi katika uwasilishaji wa tungo hizo.

Mataifa huru ya Afrika yana historia na utamaduni unaowiana. Kwa hivyo, matatizo yaliyopo katika taifa moja, ndiyo hayo yanayoshuhudiwa katika mataifa mengine ya Afrika. Katika muktadha huo, ushairi wa Kiswahili unaweza kuchukuliwa kuwa kurunzi ya kumulika matatizo yaliyopo katika mataifa hayo ya sasa. Zaidi ya hayo, watunzi hodari wa tungo hizo, walijituma na kushiriki katika utetezi wa umma. Katika kulisarifu suala hili, ithibati inatokana na mashairi yaliyohifadhiwa kwenye diwani za washairi wafuatao: A. Abdalla (1973), *Sauti ya Dhiki*; E. Kezilahabi (1974), *Kichomi*; A. Mazrui (1984), *Chembe cha Moyo*; S. A. Mohamed (2001), *Jicho la Ndani* na K. wa Mberia (2001), *Bara Jingere*.

## **2.0 Harakati za Washairi katika Kukabiliana na Matatizo katika Mataifa huru ya Afrika**

Mataifa huru ya Afrika yamekuwa yakishuhudia matatizo mbalimbali ambapo baadhi ya mashairi ya Kiswahili yamekuwa yakiyapigia kite kwa kuyabainisha au

kwa kuyabainisha na kutoa uelekezi wa kukabiliana nayo. Lengo hapa ni kuihamasisha jamii ili iweze kushiriki kikamilifu katika safari hiyo muhimu.

### **2.1 Matatizo Yaliyopo sasa katika Mataifa huru ya Afrika**

Baadhi ya matatizo ambayo yamekuwa vizingiti vya chachu ya maendeleo katika mataifa huru ya Afrika na ambayo washairi wa kiharakati wa Kiswahili wamekuwa wakiyapigia darubini kila wapatao mianya ya kufanya hivyo ni kama yafuatayo:

- Uongozi usiowajibika katika masuala ya kitaifa;
- Tatizo la ukoloni mamboleo barani Afrika;
- Viongozi wanaojitaasisisha na kuwa ‘miungu waabudiwao’ katika taifa;
- Ukiritimba unaodumaza maendeleo ya kiuchumi katika taifa;
- Utabaka unaokithiri katika maisha ya watu ndani ya jamii;
- Mielekeo na itikadi za uelekezaji kutoka mataifa ya Ulaya;
- Ukengeushi wa wanajamii kutokana na athari za tamaduni za kigeni;
- Kutozithamini taasisi muhimu zilizopo katika baadhi ya mataifa ya Afrika;
- Ukosefu wa usawa wa kijinsia katika mataifa ya Afrika;
- Kinyang’anyiro cha kuwania nyadhifa za kisiasa na athari zake;
- Ukosefu wa uhuru wa kutoa mawazo na kujieleza;
- Uhasama na ubaguzi wa kijamii kwa misingi ya ukabila na tofauti za kidini;
- Ukosefu wa uzalendo miongoni wa wananchi katika mataifa ya Afrika;
- Ufisadi uliokithiri miongoni mwa wasimamizi wa taasisi muhimu za umma; na.
- Uzohali miongoni mwa watu kuwa kizingiti au kikwazo kwa ustawi na maendeleo ya uchumi katika baadhi ya mataifa ya Afrika baada ya uhuru.

### **3.0 Sura Mbili za Harakati Muhimu Zinazotumiwa katika Ushairi wa Kiswahili**

Kimtindo, wanaharakati wa ushairi wa Kiswahili wamekuwa wakitumia lugha kwa namna mbalimbali katika uwasilishaji wa tungo hizo. Vilevile, ujumbe wa kiharakati umekuwa ukiwasilishwa kwa namna mbili: matumizi ya lugha ya moja kwa moja, na maelezo ya kitamathali au kimapumbo. Matumizi hayo ya lugha na namna ujumbe unavyowasilishwa hujenga ngome au msingi wa kiharakati katika kuihamasisha na kuizindua jamii kuhusu yanayotarajiwa kutekelezwa katika mataifa hayo ya Afrika kwa sasa.

### 3.1 Matumizi ya Lugha ya Moja kwa Moja

Ushairi wa kiharakati wa Kiswahili huweza kutumia lugha ya moja kwa moja (kwa makusudi) ili kuwasiliana na hadhira iliyokusudiwa. Katika kuelekeza, kuihamasisha na kuizindua jamii, msanii hodari wa kiharakati hufanya hivyo kwa sababu tatu. Kwanza, iwapo mazingira ya kisiasa huruhusu watu kutoa na kuwasilisha mawazo bila ya kujitia hatiani. Pili, kutokana na ujasiri, msukumo wa kizalendo na uwajibikaji katika jamii, msanii huyo huyawasilisha mawazo hayo kwa uchungu kulingana na mchomo wa hisi zake bila kujali yatakayompata. Tatu, endapo imebainika kuwa hadhira iliyokusudiwa haina ujuzi mkubwa wa kiusaili na kiutafakari kuhusu masuala hayo ya kiharakati. Kwa hivyo, inabidi kutumia lugha inayowiana na kiwango cha walengwa ili kuweza kuyaweka wazi mawazo hayo yanayowasilishwa bila utata (Achebe, 1973). Isitoshe, hapo awali mataifa ya Afrika yalipopata uhuru, asilimia kubwa ya raia wake walikuwa hawana ujuzi mkubwa wa kusoma wala kuandika. Kwa kiwango fulani hali hiyo bado ipo hata sasa. Ili kuifikia jumuiya hiyo pana, lugha inayotumiwa ni ile ya moja kwa moja ambayo haina mizungu ya kutatanisha katika upokezi wa ujumbe.

Katika miaka ya mwishoni mwa 1960 hadi 1980, baadhi ya wasanii maarufu wa fasihi kama vile Abdilatif Abdalla, Taban Lo Liyong, Kofi Awoonor, Ngugi wa Thiong'o, Micere Mugo, Katama Mkangi na Alamin Mazrui walidhibitiwa vizimbani au kuhamia mafichoni kutokana na mawazo ya kiharakati na mitazamo mikali iliyokuwapo katika sanaa zao. Hofu iliyotawala iliwafanya baadhi ya wasanii hao 'kuweka siri', kuhifadhi hisi na kuyabana mawazo yao nyoyoni au kuendelea kutunga tungo za kikasuku kwa kuendeleza itikadi za tawala zilizopo. Katika miaka hiyo, kuna wale waliojasiri; walitunga tungo zilizoweza bayana ujumbe wa kiharakati (Nyanchama, 2004; Chacha, 1980). Kwa ujasiri, baadhi ya tungo hizo za Kiswahili ziliweza kubainisha uelekezi huo kwa lugha iliyo wazi. Kwa mfano, katika shairi la 'Mnazi: Vuta N'kuvute' (*Sauti ya Dhiki*, kur. 17-22), imetongolewa:

ALII

Kwa kuwa ni haki yangu, sitahayari kuidai  
Tatumiya nguvu zangu, madhali ningali hai  
Nipate fungu langu, japo kwa ghali bei  
Nawe hapo uwe hoi (Ubeti wa 33).

Katika muktadha wa ubeti huo tunaona namna lugha ya moja kwa moja ilivyotumiwa katika kusawiri maudhui ya janja na vilinge katika upokaji wa rasilimali iliyopo katika mataifa hayo. Jambo la msingi hapa ni kuwa, jamii zimejengewa cheche za matumaini kuwa mabadiliko yanaweza kujiri pindi jitihada za ujasiri na ukakamavu zikitumika katika kuidai haki hiyo. Shime ni kwa jamii iwe na ari ya kutositisha mapambano hayo katika jamii. Hapa ieleweke kuwa, mashairi yaliyowasilisha masuala ya kijamii hayakuzishughulisha mno kalamu za

watunzi wa kiharakati. Masuala hayo ni kama vile malezi ya watoto, uzazi, mapenzi, uzingativu wa elimu katika jamii kama vile: uelekezaji wa uadilifu katika jamii, mila, imani na desturi katika jamii. Hii ni kwa kuwa baadhi ya masuala hayo yalieleweka katika mapokeo ya jamii na yamekuwa yakipigiwa debe na washairi waliotangulia. Ushairi huo wa kiharakati haukutaka kuuendeleza mjadala huo labda pale ilipobidi. Hata hivyo, masuala hayo yanapozingatiwa, huwasilishwa kwa mkabala tofauti na ule uliozoewa katika jamii. Lugha ya moja kwa moja ilitumiwa zaidi katika uwasilishaji wa ujumbe huo wa kiharakati kwa azma ya kuifikia jamii pana. Kwa hivyo, nguvu ya lugha hiyo si ya kupuuzwa kama inavyodhihirika katika baadhi ya tungo za kiharakati.

### **3.2 Lugha ya Kitamathali Kufichua na Kubainisha Matatizo Yaliyoshuhudiwa**

Lugha ya kitamathali imetumika katika ushairi wa kiharakati wa Kiswahili ili kusawiri na kufichua dhiki na uozo uliosakini zaidi katika baadhi ya mataifa ya Afrika. Kwa sababu, baadhi ya wanajamii waliuchukulia uhalisi uliowadhikisha kuwa ni majaliwa au kwa kuhofu kuyazungumzia ili kujiepusha kidole cha uchochezi au usaliti katika mataifa hayo. Lugha hiyo ya kimafumbo ilitumika mno katika kusawiri na kubainisha matatizo sugu yaliyozitutorisha baadhi ya nchi barani Afrika. Mawazo hayo yaliwasilishwa kwa lugha fiche ya makusudi na hasa ile ya mafumbo (Nzuki, 2002; Fowler, 1966). Kwa hivyo, tungo hizo ziliwasilisha mawazo hayo kitaswira, kitaashira na kiumithilishaji. Kijuuuu usawiri na uwasilishaji huo ulikuwa ni kikwazo kwa baadhi ya wasomaji kuweza kuupata ujumbe uliokusudiwa. Hadhira lengwa ya dhiti haikutindikiwa kuung'amua undani wa ujumbe uliowasilishwa. Hata hivyo, maneno au kauli zilizotumika ni zile zilizopatikana katika ushahidi wa lugha ya jamii. Kiusanii, kauli hizo huweza kushirikishwa katika uwasilishaji wa ujumbe wa kimafumbo (Wamitila, 2004; Wanyoike, 1976). Tofauti iliyopo ni kuwa, maana batini inayoibuliwa hupata mizungu ya utanuzi wa kiusaili na kiutafakari.

Kwa jicho pekuzi, matumizi ya mafumbo yamedhihirishwa pia katika baadhi ya tungo maarufu za ushairi wa Kiswahili katika karne ya 19. Kihistoria, kipindi hicho kilikuwa cha muhimu kwa wenyeji wa bara hili ambapo utawala wa ukoloni ulikuwa umekitwa katika janibu za mataifa ya Afrika. Kwa mfano, kuwapo kwa Wareno na Waarabu katika upwa wa Afrika Mashariki, kuliwachochea baadhi ya washairi maarufu kama vile Muyaka wa Muhaji kutumia lugha ya mafumbo katika harakati za kuzizindua na kuzihamasisha jamii zao kujenga mwelekeo wa kutoridhika na kutoshirikiana na tawala hizo za kigeni. Lugha hiyo ilikuwa yenye nguvu katika ubainishaji wa dhiki zilizosaki katika jamii hizo. Kwa hivyo, utumizi wa mafumbo katika uwasilishaji wa ujumbe wa kiharakati haukuwa mgeni katika utamaduni wa wenyeji. Katika kipindi cha ukoloni na miaka ya mwanzo ya Uhuru, mawazo ya kiharakati yaliwasilishwa kimafumbo ili kujenga kejeli na kinaya kuhusu tawala hizo. Kwa kufurahia uwasilishaji wa tungo hizo, watawala



au walengwa waliwatuza baadhi ya wasanii hao bila ya kutambua kuwa mambo yao yalianikwa hadharani. Mathalani, katika miaka ya 1970 Abdilatif Abdalla alituzwa na kiongozi wa kwanza wa Jamuhuri ya Kenya kwa usanifu wa tungo zake.

Katika miaka ya 1960, hasa baada ya mataifa ya Afrika kupata Uhuru, baadhi ya watawala 'weusi' walioshika hatamu za uongozi waliendeleza zaidi ngoma ya 'ubwana na utwana' kama ilivyoshuhudiwa katika enzi hizo za giza. Baadhi ya wananchi katika mataifa hayo walifikiri kuwa wamekwisha kuzikata silisili zilizowafunga; kumbe uhuru huo ulikuwa umetekwa nyara na watawala wenye 'ngozi nyeusi'. Maisha yakawa hayachukuliki na mfumo wa utawala haukuwa wenye mwelekeo uliotoka ndani bali nje ya mataifa hayo. Kutokana na mwelekeo huo, mataifa hayo hayakuweza kupiga makasia ya maendeleo ingawa yalikuwa yenye lukuki ya rasilimali asilia. Zaidi ya kubainisha uhalisia huo, washairi wa kiharakati wa Kiswahili wamezitaka nchi hizo za Afrika huru kukataa kupachikwa majina ya dharau kuwa, ni mataifa 'yanayoendelea' bali kufahamu kuwa udumazaji wa uchumi wao umeshenezewa kwao kupitia kwa aila za 'mabwana' kutoka nje kwa ushirika wa aila za 'mabwana' kutoka ndani. Wasanii waliochomoza shingo katika kubainisha uhalisi huo kupitia tungo zao, waliadhibiwa kwa virungu na kusondekwa vizimbani.

Uwasilishaji wa ujumbe wa kiharakati haukugota miamba. Tungo za ushairi wa Kiswahili zilipata shufaha ya kushaua maudhui yaliyobainisha zaidi matatizo yaliyodhikisha na kutoa uelekezi wa kuzingatia wakati wa sasa. Miongoni mwa washairi walioendeleza mikakati hiyo mwanzoni mwa miaka ya 1970 hadi 1990 ni kama vile Abdilatif Abdalla, Euphrase Kezilahabi na Alamin Mazrui. Katika miaka ya 2000 hadi sasa, mawazo hayo yaliendelezwa kwa kiwango fulani na baadhi ya wasanii kama vile S.A. Mohamed na Kithaka wa Mberia. Kimaudhui, wasanii hao wanaweza kuwekwa katika makundi mawili: wale waliostahabu kuyabainisha matatizo yaliyopo na wale waliovaa njuga siyo tu katika kuyabainisha bali pia kuyapendekezea suluhu.

Baadhi ya washairi wameweza kuziwasilisha jumuiya za Afrika kama 'zilizolala' na katu hazijatumbua mboni kuubaini uhalisi huo wala kuzumbua chanzo cha masaibu yanayowakumba. Baadhi ya taswira zinazowasilishwa katika tungo hizo ni jumuiya ambazo zimeuangamiza 'utu wao' ambao umo katika 'kifo kisichokufa'. Kadhalika, jumuiya hizo zimejidumaza na kujilemaza kutokana na mtazamo finyu kuhusu matatizo yanayozizinga. Katika muktadha huo, inaonekana kuwa baadhi ya matatizo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii hayakusukumizwa kutoka nje tu bali pia yametomelewa zaidi kupitia kwa mielekeo ya wenyeji. Kwa hivyo, suluhisho linapaswa kuzingatia uhamasishaji na uzinduzi unaotoka ndani na wala si kutoka nje. Kama vile ilivyokwisha kuelezwa, jumuiya hizo zimekuwa zikiendeleza mielekeo duni au isiyofaa katika kukabiliana na matatizo yanayoshuhudiwa. Kwa mfano, baadhi ya washairi hutoa kimako kuona jumuiya za Afrika zinavyochechemea kwa nira walizovikwa au walizojivika ilhali

zimebarikiwa kwa rasilimali tumbi na utendakazi wa jamii si wa kupigiwa mfano. Ujumbe huo umesawiriwa na kubainishwa kwenye shairi la 'Kula Njama' (*Chembe cha Moyo*, kur. 44-47), kwamba:

Si yale manoti  
Wala si mahundi  
Yapelekwayo mawindoni  
Ili kuwapandishia wala njama  
Faida iliyowashukia (uk. 46).

Ujumbe unaowasilishwa katika dondoo hilo unayalenga baadhi ya mataifa hayo ya Afrika ili kuweza kumaizi utajiri wa rasilimali uliopo ambao umenyakuliwa kwa mizungu, kinyume na uvumi unaocendelezwa na baadhi ya mataifa ya kigeni. Kwa mfano, baadhi ya mataifa ya Afrika kwa wakati wa sasa kuna rubaa kubwa ya watamba na njia ilhali mazingira hayo hayapaswi kuwapo. Kwa hivyo, wanachokipata ni kiinimacho. Kwa sababu, mataifa hayo ndiyo zalishi na migodi ya rasilimali ipo na hutumiwa kuyatajirisha na kuyaletka sifa mataifa ya kigeni (Masinde, 2003). Aidha, baadhi ya viongozi wa mataifa ya bara la Afrika hukubali (kwa kufahamu au kutofahamu) kujiingiza katika mitego ya kizungumkuti kinachotumika kuifisidi rasilimali ya mataifa hayo. Kwa hivyo, wasanii wa tungo hizo wamekuwa wenye ujasiri wa kutumia lugha ya mafumbo katika kuhoji, kusaili na kujenga mazingira ya utafakari kuhusu mikiki ya uhalisia huo kama ilivyoendelezwa katika shairi la 'Usijiangamize' (*Chembe cha Moyo*, uk. 9), kwamba:

Umekuwa ni kilema  
Kiwete tena u tasa  
Kutozaa lilo jema  
Wala dhuli kujiasa (ubeti wa 5).

Muktadha wa dondoo hilo umesawiri na kubainisha uhalisi wa maisha ya jamii na uchumi ulivyovurugwa kutokana na kipute cha nje ya mataifa hayo ya Afrika. Kutokana na mawazo hayo, umma wa mataifa ya bara hili unahitaji kuzinduliwa na kuhamasishwa, la sivyo yatabaki kwenye ulitima wa maendeleo. Wito wa uhamasishaji wa jamii katika mataifa hayo unasikika pia kupitia lugha ya mafumbo kwenye shairi la 'Afrika na Watu Wake' (*Kichomi*, uk.19), ambapo mshairi amekaulisha kauli na maelezo hayo kwa kusema kuwa:

Mimi naona mgonjwa  
Bado amelala kitandani  
Kama hatutamtoa miiba iliyobaki  
Mgonjwa hataweka miguu yake chini



Ili kutembea bila kujiegemeza (ubeti wa 1).

Mawazo hayo ya kiharakati yameibuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia taswira ya kimaono na ya kihisi ambapo masaibu yanayoyakumba na kuyayumbisha baadhi ya mataifa huru ya Afrika yamebainishwa. Hayo hayakupaswa kuwapo ingawa baadhi ya wenyeji wamekuwa wakielekeza kidole cha lawama kwa Mwenyezi Mungu bila ya kuzingatia kiini cha dhiki hizo zinazowasibu. Aidha, msanii huyo haoni mwafaka wowote kwa mataifa ya Afrika kuendelea kujizika katika tanuru hilo la kaburi. Suluhu kuhusu matatizo hayo imetolewa katika shairi la 'Usijiangamize' (*Chembe cha Moyo*, uk. 9):

Inuka mama inuka  
utoke mwako gizani  
Inuka ukilimka  
Usikike hadharani (ubeti wa 6).

Kadhalika, washairi wameonesha kukata tamaa kupitia harakati duni zinazotumika katika kutatulia matatizo yaliyopo katika baadhi ya mataifa hayo ya Afrika. Kwa hivyo, wanazitaraji jamii hizo kuibua mikakati ambayo itakuwa chachu ya kuleta matumaini ya kufikia mwafaka wa 'ndoto' iliyowaelekeza wakati walipokuwa wakishirikiana katika kupigania uhuru (Chacha, 1992). Hapo ndipo mataifa hayo yataweza kujengwa katika misingi isiyotetereka ya kimaendeleo. Shairi la 'Bara Jingere' katika (*Bara Jingere*, kur. 10-16), limedokeza baadhi ya harakati za msingi zinazoweza kuzingatiwa ili kuleta mabadiliko yanayostahili. Aidha, mataifa hayo yanahitaji kujengwa upya katika misingi ya uzalendo ambapo taasisi za umma zitawajibika na wananchi watafaidi matunda ya uhuru. Ufufuzi wa ndoto hiyo umebainishwa katika shairi lililorejelewa hapo juu, kwamba:

Bunge,  
Halitakuwa ukumbi  
Wa genge la nzige,  
"Usalama wa taifa"  
Halitakuwa ngozi  
Ya kulinda mamba wa ikulu,  
Vizuizi  
Na jela  
Hazitakuwa vinu  
Vya kusagia utu  
Mlango  
Wa kuingia kaburini  
Akili azizi  
Hazitashtuka

Na kuangusha vifaa... (kur. 10-11).

Kupitia kauli hizo zilizopigiwa mstari, mshairi ameweza kujenga taswira inayoibua ujumbe kitaashira. Katika muktadha huo, imebainishwa namna mifumo dhalimu inavyosababisha ugumu wa maisha. Kwa uelekezi zaidi wa uzinduzi wa jamii, imedhihirishwa namna 'bara hilo jingine' litakavyokuwa kupitia juhudi za wenyeji wenye mielekeo ya uzalendo. Kwa hivyo, taswira ya kimaono imetumiwa katika kufafanua namna jamii hiyo mpya itakavyonufaika kwa kuutokomeza *ufukara* ulioshamiri katika mataifa hayo. Dhana za kitaashira zilizotumika kubainisha matatizo yaliyopo ni kama vile *meno ya ufukara* na *mbwa-mwitu* anayerarua *kondoo*. Kauli hizo zimetumiwa kwa makusudi ili kuwafanya wanajamii kuelewa makali ya dhiki yanayoshuhudiwa katika baadhi ya mataifa hayo (Zubkova-Bertoncini, 2008). Isitoshe, katika shairi la 'Hatujaaga ndoto' (*Bara Jingine*, kur. 4-5) imebainishwa kwa uwazi zaidi kuathirika kwa jamii kumetokana na kutofahamu au kutozinduka kwao, kwamba:

Sumu ya kutojua  
Imefunika vijiji  
Kama ukungu wa moshi  
Kwenye njia ya msafiri ... (uk. 4).

Kwa maoni yetu ni kwamba, kundi la washairi wa Kiswahili linalowaelekeza watu kwa kuzingatia suluhu na maamuzi yafaayo ndilo la muhimu zaidi katika mataifa huru ya Afrika. Kwa sababu, huwataka wanajamii kujihusisha na kushiriki kikamilifu katika harakati za kuondoa sura zote zinazodhikisha mataifa hayo ya Afrika (Fanon, 1967; Molefi, 1999). Matokeo ya juhudi hizo ni kushuhudiwa kwa jamii yenye kuzingatia itikadi ya kimapinduzi inayojikita katika utamaduni na uhalisi wa mataifa hayo ya Afrika. Mashairi mengine yenye mwelekeo kama huo ni kama vile: 'Jicho Geni' (*Jicho la Ndani*, uk. 45); Mkombozi (*Chembe cha Moyo*, uk. 17); 'Wasafiri Tuamkeni' (*Sauti ya Dhiki*, kur. 67-72) na 'Wanafiki' (*Kichomi*, uk. 24).

**3.3 Usimulizi kama Mbinu ya Kiharakati Inayoishirikisha Jumuiya ya Watu**  
Usimulizi ni mbinu ya utambaji ambapo hushirikisha pande mbili: mwasilishaji kwa upande mmoja na mpokezi au wapokezi kwa upande mwingine. Kiungo cha pande hizo ni ujumbe unaopitishwa. Ingawa katika tungo za fasihi andishi jambo hili halijitokezi kwa uwazi, msanii huweza kutumia kunga za uwasilishaji ili kuhakikisha kuwa mbinu hiyo inadumishwa kwa kiwango fulani. Mbinu hiyo ya uwasilishaji huzingatiwa katika ushairi wa kiharakati ili kujenga muktadha wa usaili na ufasiri wa kutegemewa. Aidha, hadhira huweza kushirikishwa katika maamuzi yanayotarajiwa kuleta mabadiliko yafaayo katika jamii. Kutokana na matumizi ya kauli za nafsi ya kwanza, pili na tatu katika uwasilishaji wa tungo

hizo, washairi hao huwa na lengo la kusemezana na hadhira. Kwa mfano, shairi la 'Hadithi ya Mzee' (*Kichomi*, kur. 69-72) limewasilishwa kwa mtindo na mandhari ya utambaji kama inavyobainishwa hapa:

“Mnataka nini?”  
“Hadithi!” walijibu  
“Hadithi gani?”  
“Nzige Nzige Nzige!” (ubeti wa 2).

Katika utambaji huo, msomaji hutunga taswira ya kimaono na pia kutambua kuwa hadithi iliyotarajiwa kusimuliwa ilihusu *Nzige*. Baada ya hapo, kumejengwa mwanya wa kufaragua na kuendeleza zaidi mawazo ya kiharakati kwa kumfanya fanani kuwa kinywa cha uwasilishaji wa baadhi ya matukio muhimu yaliyopitika katika historia ya mataifa huru ya Afrika, kama ifuatavyo:

“Kwanza zilifika habari  
Habari zisizoaminika  
Kwamba huko pwani  
Kumefika wadudu  
Wadudu wenye pua ndefu  
Na walao kila wakati” (ubeti wa 4).

“Mara tukaona vimatu weusi  
Wengi wanarukaruka  
Kumbe wale nzige  
Waliacha mayai mchangani!  
Vimatu wakafufuka  
Kutoka mchangani  
Hao watoto wa nzige  
Au ni watoto wetu! ...” (ubeti wa 21).

Ujumbe unaodhihirishwa katika beti hizo ni kwamba, baadhi ya wenyeji katika mataifa ya Afrika yalipopata uhuru, walisherehekea tukio hilo ambalo lilikumbatiwa kwa mkumbo. Swali linalosailiwa hapa ni: je, juhudi hizo za wenyeji ziliweza kuufurusha kabisa mfumo wa utawala wa kikoloni? Kauli mahususi zilizotumika zimesaidia kujenga sauti ya utetezi ambapo raia wa mataifa hayo hawahitaji kutosheka na uhuru walioupata bali kuusaili na kuutathmini upya uhuru huo. Mawazo yanayowasilishwa hapa ni kuwa, wakoloni waligura kwa utashi wao baada ya kuacha athari zao kutamalaki na kuendelezwa kupitia sura nyingine (Ezeliora, 2009). Kwa mfano, wakoloni walipoondoka waliacha *mayai* ambayo yaliweza kukomaa na kuanguliwa *vimatu*. Baadaye, *vimatu* hao walikomaa kuwa *nzige* kamili ili kuendeleza udhalimu uliokuwapo. Kadhalika,

kumetumiwa viakifishi vya kufungua na kufunga usemi au unukuzi [“ ”]. Matumizi hayo huelekeza udurusu wa shairi kwa uelewa kuwa, kauli iliyotumika imetolewa na mwingine na wala si mshairi mwenyewe. Kwa hivyo, msomaji huweza kugeuza mtindo wa usomaji wa shairi ili kuweza kuakisi sauti ya mhusika mwingine. Kwa uelekezaji zaidi, kumetumiwa neno *anasema* mwishoni mwa unukuzi wa kauli halisi kama ilivyobainishwa kwenye shairi la ‘Mafahali Wapigana’ (*Kichomi*, uk. 5) ifuatavyo:

“Basi kama mchwa  
Tujenge kichuguu  
Kama mchwa tuungane  
Na kuulainisha udongo,” *anasema* (ubeti wa 3).

Katika muktadha wa dondoo hilo, uwasilishaji wa shairi umepata uelekezi zaidi kutokana na alama hiyo ya kufungua na kufunga usemi [“ ”]. Kwa kudhihirisha sauti ya shime zaidi, msanii ametumia kiakifishi cha kishangao [!]. Kwa mfano katika ubeti wa kuhitimisha shairi hilo, imetongolewa:

Patulivu! Patulivu! Patulivu!  
Lakini! Lakini! Lakini! ... (ubeti wa 4).

Katika dondoo hilo, kumekaririwa maneno mawili: *Patulivu* na *Lakini*. Katika mshororo wa kwanza, mshairi ameweza kuiga namna watazamaji walivyokuwa wakifurahia vita vya mafahali waliokuwa wakimenyana. Kwa sababu hiyo, mshairi ametilia shaka furaha hiyo, usomaji unaelekezwa kwa alama ya kishangao katika udodoso wa maneno yaliyotumika kama inavyodhihirika katika: *Patulivu!* na *Lakini!* Kadhalika, maneno hayo hayakurudiwa tu holela kama mbinu ya ukariri na udhibiti wa mahadhi na ridhimu bali pia kama njia ya kuushadidia zaidi ujumbe wa kiharakati katika shairi hilo. Isitoshe, kauli hizo zinazotumika kwa hadhari ili kujenga maingiliano ya pande mbili: mwasilishaji na hadhira kusudiwa (Njogu, 1993; Austin, 1962). Zaidi ya uwasilishaji wa ujumbe, msanii ameweza kujenga muktadha wa kusemezana kwa ubunifu na hadhira. Kwa maana hiyo, ushairi wa kiharakati hujibainisha kwenye usemezano unaounganisha pande mbili kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali. Katika mazingira hayo, akili ya wasomaji hujengewa uelekezo wa kutathmini na utafakari wa ujumbe unaowasilishwa katika tungo hizo. Mfano mwingine unaoweza kutumika ni ‘Mruko wa Nyuki’ (*Bara Jingine*, kur. 20-25).

### 3.4 Ufupi na Urefu wa Tungo za Ushairi wa Kiharakati wa Kiswahili

Ushairi wa kiharakati huweza kushirikisha ubeti mmoja au zaidi lakini ni mkufu wa mawazo yanayowasilishwa kipicha, kiistiari na kimafumbo. Tungo hizo huwasilisha lukuki ya mawazo kwa muhtasari unaozingatia uhalisi mchungu unaoshuhudiwa katika mataifa ya Afrika. Mfano hapa ni kama inavyobainika

katika shairi la 'Machizi ya Damu' (*Bara Jingere*, uk. 1); 'Karamu ya Kadimu' (*Jicho La Ndani*, uk. 82) na 'Jana Leo na Kesho' (*Chembe cha Moyo*, uk. 42). Ingawa baadhi ya mashairi huwasilishwa kwa ubeti mmojammoja; maelezo ya kina huhitajika kufafanulia matini za kitaashira na kisitiari (Senkoro, 1988). Huo ni ustadi unaotumika katika kuishirikisha hadhira kujaziliza maelezo yaliyobaki. Hilo pia huzingatiwa katika muktadha wa idadi za beti zilizoshirikishwa ambapo hoja muhimu huashiriwa kiawamu. Ubainishaji huo hutokana na tajiriba ya mtunzi kwa kuzingatia mpekecho wa hisi alizonazo. Kwa kufanya hivyo, washairi huitaka jamii kujenga taswira ya kuwabaini wahujumu wa uchumi na maendeleo katika mataifa hayo.

Masuala ya msingi ya kiharakati huhitaji kutolewa viashiria vya usuli unaokubalika katika jamii. Kwa mfano, mfumo wa utawala uliopo umekuwa ukishirikisha viongozi ambao wameyafanya mataifa hayo kuwa himaya au *nyumbani* mwao. Hiyo ndiyo sababu ya hoja hizo kuashiriwa kwa kauli za kimapumbo na kisitiari kwenye shairi la 'Bara Jingere' (*Bara Jingere*, kur. 10-16). Kwamba, mataifa hayo:

...Ambamo nyati  
Amekumbwa na ghadhabu  
Mbwa-mwitu  
Wanateketezwa na kichaa  
Swila  
Amefurisha shingo (uk. 11).

Taswira iliyojengwa kupitia kauli zilizotumika katika dondoo hilo ni kwamba, mataifa hayo ya Afrika yameshuhudia vurugu za kisiasa na tafrani za kiuchumi ambapo usalama wa kitaifa haujapewa kipaumbele. Kisemiotiki, kauli teule zinazotumika katika tungo za kifasahi huwa zinahitaji kufasiriwa kwa kuzingatia utamaduni, uhalisi wa maisha na historia katika jamii husika (Fowler, 1966). Kwa sababu, baadhi ya viongozi hujifanya miungu ya kuwanyanyasa na kuwatatiza watu katika nyanja zote za maisha. Kadhalika, imekaririwa zaidi kuwa mataifa hayo yamevikwa nira na kutekwa nyara kiuchumi na kisiasa. Kilio cha wasanii kama inavyoelezwa katika shairi hilo la Wa Mberia (*keshatajwa*) ni kuwa, kuna umuhimu wa mataifa huru ya Afrika kujizatiti na kupania ukombozi wa pili ambapo masuala ya msingi yatapelewa kipaumbele. Ukombozi huo wa pili utakaposhuhudiwa, mataifa hayo yataweza kujengwa katika misingi madhubuti kama inavyoelezwa hapa:

Ulafi  
Na ufiadi  
Hazitanyesha kutoka juu  
Urongo rasmi

Hautapaa angani  
 Ubaguzi wa kikabila  
 Hautakuwa ukungu  
 Katika ikulu  
 Hakutapinda mamba  
 Bali kuketi binadamu  
 Watu wenye damu  
 Na fahamu... (kur. 11-12).

Kimsingi, msanii wa tungo za kiharakati huwa hana muda mwingi katika ufaraguzi: mawazo huwasilishwa kwa kudokezwa. Hata pale ambapo beti zaidi hutumika, mtunzi hakuwa na budi kuepuka. Aidha, hadhira hutarajiwa kuchangia katika kutoa mifano na maelezo yanayoakisi ujumbe unaowasilishwa. Isitoshe, hadhira hujengewa muktadha wa kujumuishwa katika harakati hizo za kuleta mabadiliko (Njogu, 2004). Katika muktadha huo hakuna atakayejigamba kuzihodhi juhudi hizo. Baadhi ya kauli zinazotumika hujenga usaili na utafakari ni kama inavyobainika katika shairi la 'Kula Njama' (*Chembe cha Moyo*, kur. 44-47), kwamba:

Tuna haja ya shaka, dada zangu?  
 Shaka hatuna haja nayo.  
 Tuna haja ya utafiti ndugu zangu?  
 Utafiti hatuna haja nao (uk. 45).

Dondoo hilo ni miongoni mwa mishororo muhimu katika shairi, ambapo umeufundika na kuusetiri ujumbe wa kiharakati wenye lengo la kujenga mazingira ya uzinduzi miongoni mwa jamii za mataifa ya Kiafrika kwa wakati wa sasa. Kwamba, dhiki zilizopo ni ithibati tosha ya machungu katika mataifa hayo. Kilichobaki ni hadhira kuchukua hatua ya kuleta mabadiliko. Mawazo yanayopitishwa kwa muhtasari huwa ni kivutio kikuu kwa hadhira ambapo huupata ujumbe bila kutumia muda mwingi katika udurusu. Muda wa ziada huweza kutumiwa katika kutafakari na kusaili ili kujenga mikakati inayopaswa kuzingatiwa. Kutokana na vichujio vya mkururo wa mawazo, kiini cha ujumbe husaki akilini kwa wakati uliopo na pia kwa wakati ujao. Huo ni msingi wa kuelekeza kutathmini jamii kwa kizazi kilichopo kwa sasa na kijacho. Ni katika hali hiyo ambapo mtunzi hujengea hadhira muktadha wa marejeleo hasa kwa kuzingatia kauli teule zilizotumika kuwasilishia mawazo hayo ya kiharakati katika tungo hizo.

#### 4.0 Hitimisho

Makala haya yamefafanua namna ushairi wa kiharakati wa Kiswahili unavyotumiwa kubainishia baadhi ya matatizo sugu yanayoshuhudiwa kwa sasa katika mataifa huru ya Afrika. Aidha, ujumbe wa kiharakati huwasilishwa kupitia



maudhui yanayosawiriwa na pia kupitia namna lugha ilivyotumiwa. Katika misingi hiyo, ushairi wa Kiswahili umetumika kuwa chombo cha kubainishia hali iliyopo na pia katika kuelekeza juhudi zinazopaswa kuzingatiwa ili kuizumbua ndoto ya matumaini katika mataifa hayo. Kwamba, ustawi wa taifa ni utaifa wake, haki na usawa wa watu wake. Swali ambalo limekuwa likishughulikiwa na washairi hao ni kuwa: uhuru ambao unashuhudiwa kwa wakati wa sasa Afrika ni kamili? Je, raia hao wanapaswa kuchukua hatua gani katika kusawazisha dosari iliyopo? Mwelekeo unaojengwa katika tungo hizo huwaelekeza wanajamii kujiamini na kuhamasishana wao kwa wao ili kujenga ngome imara ya kukabiliana na matatizo sugu yanayolemaza maendeleo katika mataifa hayo. Hiyo ni safari ambayo kila mwananchi anapaswa kujiandaa nayo. Ingawa tungo hizo ni muhimu, wito ni kwamba, hazipaswi tu kuhifadhi uhalisia mchungu unaoshuhudiwa Afrika kwa wakati wa sasa. Tungo hizo za kiharakati zinapaswa kughaniwa hadharani katika hafla rasmi na zile zisizo rasmi. Kwa kufanya hivyo, nguvu na athari yake itahisika katika jamii pana ya mataifa hayo. Aidha tungo hizo zinaweza kutolewa kwa hadhira ambapo jamii itakuwa inahisi kuhusishwa kikamilifu kuleta suluhu ya kurekebisha dosari zilizopo katika mataifa hayo. Hayo yakapokumbatiwa ndipo mwenge wa ndoto ya matumaini uliokuwapo kabla ya uhuru na kuzongwa kwa wakati wa sasa utashajiishwa ili kuwa chachu ya dhati katika kupania ukombozi wa pili katika mataifa hayo.

### Marejeo

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abdalla, A. (1978). 'Wajibu wa Mshairi wa Kiswahili katika Jamii yake' Katika *Zinduko*. Dar es Salaam: Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Achebe, C. (1973). 'The Novelist as a Teacher' Katika Killam, G. D. (Mh.) *African Writers on African Writing*. London: Heinemann.
- Austin, J. (1962). *How to do Things with Words*. Clarendon: Oxford University Press.
- Chacha, C. N. (1980). "Ushairi wa Abdilatif Abdalla", Tasinifu ya M.A. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi
- Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utezezi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Ezeliora, O. (2009). 'Colonial Discourse, Poetic Language and the Igbo Masquerading Culture in Ezenwa Ohaetos: The Voice of the Night Masquerade', Katika *Journal of African Cultural Studies*, Juzuu 21 na. 1. London: SOAS.
- Fanon, F. (1967). *Black Skins, White Masks*. New York: Grove Press.

- Fowler, R. (1966). "The Formulaic Theory and its Application to English Alliterative Poetry", katika Fowler, R. (Mh.), *Essays on Style and Language*. London: Routledge & Kegan.
- Gromov, M. D. (2006). 'The Question of Kiswahili Style Again? The Poetry of Kithaka wa Mberia' katika *Kiswahili* Juzuu 69. Dar es Salaam: TUKI.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.
- Khatib, M. S. (1999). 'Tamathali za Usemi' katika *Mulika* Juzuu la. 25. Dar es Salaam: TUKI.
- Masinde, E. (2003). "Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui," Tasnifu ya Ph.D. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Matheka, B. (2013). 'Wakenya Wangoja Uhuru wa Kweli' Katika *Taifa Leo*, Novemba 12, 2013. Nairobi: Nation Media Group Ltd.
- Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.
- Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa*. Nairobi, Educational Research and Publications.
- Mohamed, S.A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishes (K) Ltd.
- Molefi, K. (1999). *The Painful Demise of Eurocentricism*. Trenton: N.J, African World Press Inc.
- Mulokozi, M. M. (1978). 'Ushairi na Ukasuku', Katika *Kioo cha Lugha*. Dar es Salaam.
- Mwachilumo, P. (2013). 'Tatizo la Ukoloni Mamboleo Barani Afrika' Katika *Taifa Leo*, Novemba 29, 2013. Nairobi: Nation Media Group. Uk. 23
- Njogu, K. (1993). "Dialogic Poetry: Contestation and Social Challenge in East African Poetic Genres." Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa).
- Nyanchama, M. B. (2004). "Matumizi ya Taswira na Istiara katika *Sauti ya Dhiki*," Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Nzuki, P. K. (2002). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia." Tasnifu ya M.A.. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Ohly, R. (1973). 'Historical Approach to Swahili Literature As Here to Fore an Open Question' Katika *Kiswahili* Juzuu Na. 43/2. Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Wa Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publication Ltd.
- Wamitila, K. W. (2002). 'Utangulizi' Katika Mohamed S. A. *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn (Kenya) Ltd.
- Zubkova-Bertoncini, E. (2008). 'Some Remarks on Kithaka wa Mberia's Poetry' Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la 21<sup>st</sup> Century Swahili-Kolloquium, Chuo Kikuu cha Bayreuth.